

THE JOMO KENYATTA FOUNDATION

M KATABA WA HUDUMA KWA WATEJA

AZMA

Kutoa huduma za kitaaluma katika uchapishaji wa vitabu na ufadhili wa wanafunzi werevu wa shule za upili wasiojiweza kifedha. Taasisi hii inajizatiti kutunza na kutosheleza wateja wake na wengine wanaonufaika kutohakana na taasisi hii.

AHADI YETU

Uongozi

Tutawajibika katika matendo yetu na kuwa mfano mwema.

Utunzaji

Tunawatunza wateja wetu.

Ushirikiano

Tutafanya kazi pamoja kwa ari na shauku.

Afya na usalama

Tunawajibika katika kudumisha mazingira salama ambapo tunajali hali njema ya kila mtu.

Uaminifu na uadilifu

Tunafanya shughuli zetu kwa uaminifu na uadilifu.

Jamii

Tunatambua wajibu wetu katika jamii na mazingira. Hivyo, tunafanya shughuli zetu kwa uangalifu na kwa kuzijali jamii zinazotuzunguka.

Bidhaa na huduma

Tutatoa uchapishaji bora, bidhaa na huduma za ufadhili ambazo zitapiku mahitaji ya wateja wetu.

• *Uchapishaji*

Tutajitahidi hasa kuwawezesha waandishi kupata huduma zetu za uchapishaji wa kitaaluma kwa urahisi ili kuhakikisha kuwa machapisho yetu yanaridhisha matakwa ya wateja.

• *Ufadhili*

Tutatoa huduma bora zaidi za ufadhili kwa wanafunzi werevu wasiojiweza kifedha katika jamii ya wakenya.

Malalamishi

Ikiwezekana, malalamishi yatashughulikiwa punde tu baada ya kuwasilishwa. Hata hivyo, ikiwa haiwezekani kushughulikia malalamish hayo hapohapo, yatasuluhishwa na anayehusika kabla ya wiki 3 kupita.

HAKI ZA MTEJA

Maoni

- Mawasiliano yatajibiwa kabla ya siku 21 za utenda kazi.
- Nyaraka za elektroniki(imeli) zitajibiwa kabla ya saa 48 kupita.
- Simu zote zinazopigwa wakati wa kazi zitajibiwa kufikia mara ya tatu. Atakayechukua simu atajitambulisha kabla ya kuendelea na maongezi.

Bidhaa na huduma bora

Wateja wetu watapata huduma na bidhaa bora kwa bei nafuu.

Sifa na malalamishi

Wateja wanahimizwa kutoa malalamishi, mapendekezo na sifa zinazohusiana na bidhaa zetu na utoaji wa huduma. Mteja ana haki ya kujua afisa anayemhudumia.

Usiri

Wateja wetu wataheshimiwa na mambo yao yatashughulikiwa kwa usiri sana.

Mkataba huu unafanya kazi na utarekebishwa kila baada ya muda kulingana na mwelekeo wa biashara. Utatathminiwa kila mwaka kwa minajili ya kuendelea kujiboresha. Matokeo ya utathmini huo yatachapishwa na washika dau wote wataweza kupata matokeo hayo.

HUDUMA ZETU ANUWAI

HUDUMA	MAHITAJI	BEI	MUDA WA KUSHUGHULIKIWA
Uchapishaji	Uwasilishaji wa mswada uliochapwa	Hakuna malipo	Muda unaokubalika
Uuzaji wa vitabu na bidhaa zingine za mafunzo		Angalia bei katika <i>Orange Book</i>	Haraka iwezekanavyo
Uhariri wa Nyaraka	Kielelezo cha mteja (<i>soft copy</i>)	Kshs 150 kwa kila ukurasa	Muda unaokubalika
Kupiga chapa na kusanifu maandiko ya kawaida	Kielelezo na maagizo ya mteja	Kshs 250 kwa kila ukurasa	Muda unaokubalika
Kupiga chapa na kusanifu maandiko ya sayansi na hesabu	Kielelezo na maagizo ya mteja	Kshs 1000 kwa kila ukurasa	Muda unaokubalika
Usanifu wa jalada	Maagizo ya mteja	Kshs 10,000	Siku tatu za kazi
Usanifu wa nembo	Maagizo ya mteja	Kshs 20,000	Siku saba za kazi
Usanifu wa kadi za arusi na kadi za kuchangisha pesa	Kielelezo na maagizo ya mteja	Kshs 500	Siku tatu za kazi
Usanifu wa cheti	Kielelezo na maagizo ya mteja	Kshs 3,000	Siku tatu za kazi
Usanifu wa kadi biashara na vijikaratasi vya salamu	Kielelezo cha mteja	Kshs 3,000 kwa kila moja	Siku tatu za kazi
Kuchanganua(kwa ajili ya kutumika kwa kazi yoyote ya usanifu)	Picha/Michoro	Kshs 650 kwa kila mchoro	

NAMBA RI ZA MAWASILIANO

THE JOMO KENYATTA FOUNDATION	OFISI KUU: 020 2329987, 020 2330002/3, 6536200/1/2. Rununu: 0723 286993, 0723 969793, 0735 339135. TAWI LA KIJABE STREET: 0208155454, 0721136413, 0735136413. Baruapepe: info@jkf.co.ke Tovuti: www.jkf.co.ke
COMMISSION ON ADMINISTRATIVE JUSTICE	WESTLANDS TOWERS, Ghorofa ya Pili, WAIYAKI WAY, WESTLANDS • S.L.P. 20414 – 0200 NAIROBI • Rununu: +2540202270000 Simu ya Dharura: 00800221349 Nambari ya Ujumbe fupi: 15700 • Tovuti: www.ombudsman.go.ke